SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# AFISI YA RAIS IKULU

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI
## AFISI YA RAIS IKULU
## MHESHIMIWA JAMAL KASSIM ALI

---

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

---

APRILI, 2022

## YALIYOMO

1. ORODHA YA VIAMBATISHO ..................................... iii
2. VIFUPISHO VYA MANENO ....................................... iv
3. UTANGULIZI .................................................................. 1
4. MAJUKUMU YA AFISI YA RAIS IKULU ........................ 3
5 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA AFISI YA RAIS IKULU KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2021/2022 ................................ 7
6. MWELEKEO WA BAJETI YA AFISI YA RAIS IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ....................... 39
7. PROGRAMU KUU NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA ZINAZOHITAJIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 .............................................. 40
8. MAMBO MAKUU YATAKAYOTEKELEZWA NA AFISI YA RAIS IKULU KWA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023 ........................................................... 50
9. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ................................................................... 50
10. HITIMISHO ................................................................... 51

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Nam. 1. Mchanganuo wa Maagizo kwa kila Mkoa. ........................................................................ 53

Kiambatisho Nam. 2. Orodha ya Mada zilizojadiliwa kupitia Televisheni na Redio katika kipindi cha “Unatekelezaje? kwa kipindi cha Julai 2021 - Machi 2022. .................................................... 54

Kiambatisho Nam. 3. Idadi ya taarifa zilizorushwa na waliotembelea Tovuti ya Ikulu kwa Kipindi cha Miezi Tisa 2021 – 2022 ........................................................ 60

Kiambatisho Nam. 4. Taarifa zilizorushwa Kupitia Mitandao ya Kijamii ya Ikulu kwa Kipindi cha Miezi Tisa 2021 – 2022. ................................................................ 61

Kiambatisho Nam. 5. Orodha ya Malalamiko yaliyowasilishwa na Wananchi kwa Kipindi cha Miezi 9 kutoka Julai mpaka Machi 2021/2022. ...................63

Kiambatisho Nam. 6. Takwimu za Malalamiko yaliyowasilishwa na Wananchi kwa Taasisi 45 za Serikali zilizounganishwa katika Mfumo wa Sema na Rais kwa Kipindi Julai – Machi 2021/2022. ......................... 64

Kiambatisho Nam. 7. Idadi ya Taasisi na Watumishi waliopatiwa Semina ya Utunzaji Nyaraka na Udhibiti wa Siri za Serikali. ................................................... 68

Kiambatisho Nam. 8. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Kazi za Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023. .............................................................. 69

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AfCFTA | Afirca Continental Free Trade Area (Soko huru la Biashara la Nchi za Afrika) |
| AMREF | African Medical and Research Foundation (Shirika la Utafiti wa Madawa Afrika) |
| AU | African Union (Umoja wa Nchi za Afrika) |
| BLM | Baraza la Mapinduzi |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| COMESA | Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja za Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika) |
| DRC | Democratic Repulic of Congo (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) |
| EAC | East Africa Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| GSO | Government Security Office (Afisi ya Usalama wa Serikali) |
| IORA | Indian Ocean Rim Association (Jumuiya za Nchi zilizopakana na Bahari ya Hindi) |
| JCC | Joint Commission for Cooperation (Tume ya Pamoja ya Ushirikiano) |
| JPC | Joint Permanent Commission (Tume za Kudumu za Pamoja) |
| KBLM/KMK | Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi |
| NTB's | Non-Tariff Barriers (Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru) |
| SADC | Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika) |
| SDG's | Sustainable Development Goals (Malengo ya Maendeleo ya Melenia) |

| | |
|---|---|
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SNR | Sema na Rais |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TZS | Tanzania Shiling (Shilingi ya Kitanzania |
| UAE | United Arab Emirates (Umoja wa Falme za Kiarabu) |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNICEF | United Nations International Children's Emergency Fund (Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto) |
| USD | United State Dollar (Fedha ya Marekani) |
| UWEMAJO | Umoja wa Wenye Mashamba Jozani |
| VVU/UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan 2021 - 2026 (Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar) |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority (Mamlaka ya Maji Zanzibar) |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation (Shirika la Utangazaji la Zanzibar) |
| ZCTV | Zanzibar Cable Television |

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kukutana hapa katika kikao hiki muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Aidha, kwa namna ya pekee namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kwa mara nyengine tena na kunipa jukumu la kuhudumu katika Afisi yake. Vile vile, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuongoza, kutuelekeza na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa majukumu ya Serikali kama ilivyoainishwa katika Katiba, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026 (ZADEP) na Mipango mikuu ya Maendeleo kwa Taifa letu.

2. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoiongoza Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi na kusimamia vyema Miradi mikubwa ya kimkakati katika kipinbdi cha mwaka mmoja cha uongozi wake. Aidha sisi sote ni mashahidi tunaona namna anavyoifungua nchi katika diplomasia ya uchumi.

3. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla, Makamu wa Pili wa Rais kwa namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majuku yake ya kila siku ya kuongoza na kusimamia shughuli za serikali.

4. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na naibu wako Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Mwenyekiti wa Baraza lako Tukufu Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma kwa kuliongoza vyema Taifa hili. Katika uongozi wako tumeshuhudia uendeshaji wa mijadala iliyo wazi na yenye nidhamu ya hali ya juu ya waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako.

5. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukran maalum kwa Mwenyekiti wa kamati ya kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mheshimiwa Machano Othman Said Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf, Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa mashirikiano na miongozo wanayotupatia.

6. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu imeanzishwa kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa Mheshimiwa Rais katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu namba 50(04). Afisi ya Rais Ikulu ni matokeo ya mabadiliko ya Miundo ya

Wizara yaliyofanyika mara tu baada ya kuanza kwa Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Awali Afisi hii ilikuwa ni sehemu ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na mnamo tarehe 10 Julai, 2021 ilianzishwa Afisi ya Rais Ikulu.

7. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu katika Awamu hii ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeundwa upya na kuongezewa majukumu ya kushughulikia Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar. Kwa sasa, Afisi ya Rais Ikulu ina jukumu la kusimamimima Afisi ya Faragha ya Mheshimiwa Rais, Afisi ya Baraza la Mapinduzi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mawasiliano na Habari, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi, Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO), Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu na Afisi ya Rais Ikulu - Pemba.

## MAJUKUMU YA AFISI YA RAIS IKULU

8. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mabadiliko yaliyofanyika Serikalini, Afisi ya Rais Ikulu itatekeleza majukumu yafuatayo:
   i. Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
   ii. Kuhakikisha kuwa jamii inapata habari juu ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo na Sera zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais

wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

iii. Kusimamia majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.
iv. Kusaidia uchambuzi wa Nyaraka na Sheria zinazotarajiwa kuwasilishwa serikalini pamoja na kufuatilia utekelezaji wake.
v. Kuratibu na kusimamia shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora).
vi. Kuratibu na kuandaa shughuli za Mipango, Sera na Utafiti katika Afisi ya Rais Ikulu.
vii. Kusimamia Nyaraka na Kumbukumbu zote za Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kwa zile Taasisi zake zilizopo Zanzibar.
viii. Kupanga na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi ya Usalama wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (GSO).

9. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba uniruhusu niwasilishe kwa ufupi Utekelezaji wa Programu za Afisi ya Rais Ikulu kwa kipindi cha Julai 2021 – Machi 2022.

10. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilitekeleza Programu kuu tano na ndogo 14 chini ya Mafungu mawili ambayo ni A01 na A02. Utekelezaji wa Programu hizi, ulizingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 - 2025, ZADEP, Hotuba ya Rais wa Zanzibar

na Mwenyekiti wa Bararaza la Mapinduzi aliyoitoa katika ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi pamoja na miongozo, maelekezo na maagizo aliyoyatoa. Kupitia Programu zake, Afisi iliandaa Mpango Kazi wa mwaka 2021/2022 na kuweka vipaumbele katika mambo yafuatayo:-

a) Kuimarisha utendaji na umakini katika matumizi ya rasilimali za Serikali

11. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuhimiza umakini katika nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kupiga vita vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi. Ni imani yetu kuwa, umma na wadau wa maendeleo wameshuhudia utumishi unaofuata sheria na uadilifu katika kuhudumia jamii pamoja na kuimarika kwa nidhamu za watendaji wa Serikali. Aidha, pamoja na mabadiliko hayo, Serikali inaendelea kuwahimiza watendaji wa Wizara, Idara na Taasisi zake kuzingati sheria na uwadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao ili kupata matokeo ya utumishi wenye ufanisi.

b) Kudumisha Amani na Utulivu Nchini

12. **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia ziara na mikutano yake na makundi mbali mbali ya kijamii, ameendelea kuhimiza umuhimu wa kudumisha

amani na utulivu. Kwa kutolea mfano tarehe 25 Machi, 2022 wakati alipokuwa akizungumza na waumini wa dini ya kiislamu katika Masjid Arafa Mombasa Wilaya ya Magharibi “B” aliwasisitiza wananchi kuendelea kuhubiri amani.

c) Kuimarika kwa Ushiriki wa Zanzibar katika masuala ya Mtangamano wa Kikanda na Jumuiya za Kimataifa

13. **Mheshimiwa Spika,** Afisi kupitia Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi, imehakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na uhusiano wa Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Katika kufikia hatua hii, wataalamu wamewezeshwa kushiriki katika vikao vya mtangamano wa kikanda na kimataifa, pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa na faida zinazotokana na Jumuiya hizo. Aidha, Serikali inaendelea kuzihamasisha balozi na jumuiya za kimataifa kufungua Afisi ndogo za uwakilishi Zanzibar ili ziweze kiungo muhimu cha kukuza uwekezaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa katika nchi zao na kuvutia uwekezaji Zanzibar.

d) Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi.

14. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu imeweka mazingira wezeshi na kuendelea kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) ili waweze kuzitangaza

fursa zinazopatikana nchini na kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu. Afisi imehakikisha kuwa, kupitia sheria namba 4 ya 2020, inayosimamia utekelezaji wa Sera ya Diaspora kwa mujibu wa miongozo iliyopo imewezesha wanadiaspora wa Zanzibar kushiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

e) Kusimamia na Kutunza Nyaraka na Kumbukumbu.

15. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu, kupitia Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu imeendelea kufanya ukaguzi wa kumbukumbu na nyaraka kwa Wizara na Taasisi za Serikali. Aidha, imeweza kutoa huduma za utafiti kwa Watafiti wa ndani na Watafiti nje ya nchi. Vile vile Afisi imetangaza na kutoa taaluma kuhusu kazi, majukumu na umuhimu wa nyaraka zinazohifadhiwa na Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar kupitia Maonesho ya Biashara ya kuadhimisha Sherehe za Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA AFISI YA RAIS IKULU KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2021/2022

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Afisi ya Rais Ikulu kupitia Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu ilipangiwa kukusanya TZS. 15.0 Milioni.

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Fungu A01 lilitengewa jumla ya TZS. 12,465.0 Milioni. Kati ya hizo TZS. 6,000.0 Milioni kwa ajili ya Mradi wa Maendeleo na TZS. 6,465.0 Milioni kwa ajili ya Kazi za Kawaida na Fungu A02 lilitengewa jumla ya TZS. 2,194.5 Milioni kwa ajili ya Kazi za Kawaida.

18. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilijipangia kutekeleza Programu Kuu sita (6) na Programu ndogo kumi na mbili (12) kupitia Fungu A01 - Afisi ya Rais Ikulu na Fungu A02 - Afisi ya Baraza la Mapinduzi. Kupitia utekelezaji huo Afisi imepata mafanikio yafuatayo: -

## MAFANIKIO YA FUNGU A01

1. **Programu Kuu ya Kusimamia na Kuratibu Shughuli na Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu.**

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 3,977.9 Milioni kwa matumizi ya Kazi za Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 programu hii iliingiziwa jumla ya TZS. 2,169.7 Milioni sawa na asilimia 54 kwa matumizi ya Kazi za Kawaida.

20. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii umepelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais kukutana na wageni mbali mbali wakiwemo

mabalozi, watu mashuhuri pamoja na wawekezaji ambao wameonesha nia ya kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi kupitia uwekezaji wanaoweza kuufanya hapa Zanzibar. Aidha, umeuwezesha Umma na wadau wote kwa ujumla kuwa na uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais.

21. **Mheshimiwa Spika,** Katika kufanikisha Uratibu wa shughuli za Mheshimiwa Rais ndani ya kipindi cha miezi tisa, Afisi ilisimamia masuala mbali mbali pamoja na kufanya vikao na watendaji wa Taasisi na wageni wa nje na ndani waliofika Ikulu kuonana na Mheshimiwa Rais. Vikao hivyo vya watendaji wa Taasisi za Serikali vilihusisha zaidi maelekezo na kutoa taarifa za utekelezaji wa kazi ambazo Taasisi hizo zilipewa kuzitekeleza. Aidha, Mheshimiwa Rais alikutana na wawekezaji waliofika Ikulu kwa lengo la kubainisha dhamira zao za kuwekeza Zanzibar katika sekta za maendeleo ikiwemo Viwanda, Utalii, Miundombinu, Ujenzi, Mawasiliano, Elimu na Afya.

22. **Mheshimiwa Spika,** Katika kukuza na kuendeleza ushirikiano na Diplomasia, Mheshimiwa Rais alikutana na Mabalozi na Viongozi kutoka Mataifa mbali mbali na Jumuiya za Kimataifa waliofika Ikulu. Miongoni mwao Mabalozi hao ni Balozi wa India, Uingereza, China, Japan, Itali, Marekani, Uswiswi na, Sweden. Aidha alikutana na wawakilishi wa Jumuiya za kimataifa kama ile UNDP, World Bank, UNICEF, Tony

Blair Foundation, UNICEF na AMREF. Katika majadiliano yao Mheshimiwa Rais alieleza haja ya kuendeleza ushirikiano uliopo kwa faida za pande zote na alishukuru kwa mchango unaotolewa na nchi na Jumuiya hizo kwa Zanzibar na Tanzania.

23. **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Rais alikukutana na Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi za nje. Miongoni mwao Prof. Adelarous Kilangi Balozi wa Brazil, Pereira Ame Silima Balozi wa Commoro, Said Shaib Mussa Balozi wa Kuwait, Fredrick Ibrahim Kibuya Balozi wa Urusi, Said Juma Mshana Balozi wa DR Congo. Katika nasaha zake kwa Mabalozi hao aliwasisitiza haja ya kuimarisha diplomasia ya uchumi na kuzitangaza fursa mbali mbali ambazo nchi yetu inazo hasa katika uchumi wa buluu na biashara.

24. **Mheshimiwa Spika,** Afisi pia imeweza kuratibu kwa mafanikio ziara za Mheshimiwa Rais zikiwemo ziara za ndani alizozifanya katika Wilaya zote za Unguja na Pemba tarehe 03 Julai hadi 03 Septemba 2021. Katika ziara hizo, Mheshimiwa Rais alitembelea na kukagua miradi mbali mbali ya maendeleo na kusikiliza changamoto zinazowakabili wananchi katika maeneo yao zikiwemo ukosefu wa huduma za maji safi na salama, uvuvi, elimu, huduma za afya na umeme, migogoro ya ardhi, changamoto za wajasiriamali pamoja na barabara. Nyengine ni wizi wa mazao na mifugo na matumizi ya madawa ya kulevya. Kufuatia changamoto zilizobainishwa na wananchi, Mheshimiwa Rais alitoa maagizo

kwa Taasisi zinazohusika kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo.

25. **Mheshimiwa Spika,** kupitia ziara zilizofanywa katika Mikoa na Wilaya zote za Unguja na Pemba, Mheshimiwa Rais ametoa maagizo katika sekta mbali mbali. Katika kuhakikisha utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa, Afisi ya Rais Ikulu inaendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo. Kwa kipindi cha Julai 2021, hadi Machi, 2022 maagizo 50 yametekelezwa ambayo ni sawa na asilimia 82.0 ya utekelezaji. **Mchanganuo wa maagizo kwa kila Mkoa unapatikana katika kiambatisho Nam. 01**

26. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeratibu ziara moja ya Mheshimiwa Rais aliyoifanya katika Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu kuanzia tarehe 17 - 19 Januari, 2022. Ziara hio ilitokana na Mwaliko aliyopewa na Mheshimiwa Sheikh Mohammed Bin Zayed Al Nahyan, Mrithi wa Mfalme wa Abu Dhabi ambae pia ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Umoja wa Falme za Kiarabu. Mualiko huo ulimuezesha Mheshimiwa Rais kushiriki kwenye ufunguzi wa wiki ya Mendeleo endelevu ya Abu Dhabi na utoaji wa Tuzo za Zayed Future Energy Prize Awards.

27. **Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo Mheshimiwa Rais na ujumbe wake walipata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi mbali mbali wa Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu na Viongozi wa Makampuni makubwa ya uwekezaji

ya Umoja wa Falme za Kiarabu. Vile vile, alikutana na kufanya mazungumzo na wafanya biashara wakubwa pamoja na kutembelea Banda la Tanzania kwenye Maonesho ya Dunia ya Dubai Expo 2020.

28. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio yaliyopatikana kutokana na ziara hiyo, ni pamoja na kukaribisha uwekezaji nchini katika sekta mbali mbali zikiwemo za utalii, ujasiriamali, biashara, barabara, afya, mafuta na gesi asilia. Aidha, ziara hiyo imeimarisha uhusiano kati ya Zanzibar na nchi za Falme za Kiarabu. Katika mazungumzo yake ya tarehe 17 Januari, 2022 na Mwekezaji wa majengo marefu ya biashara Bwana Jean Paul Cassia. Mwekezaji huyo alieleza dhamira yake ya kujenga Jengo refu zaidi Afrika ya Mashariki hapa Zanzibar. Bwana Cassia alimueleza Mheshimiwa Rais kuwa, tayari amekamilisha mchoro na andikio la jengo hilo ambalo litajengwa Mji Mkongwe na yupo kwenye majadiliano na wawekezaji kutoka China ambao wameonesha kuwa tayari kutoa fedha za kuendeleza mradi huo.

29. **Mheshimiwa Spika,** Tarehe 17 Januari, 2022 Mheshimiwa Rais alishuhudia utiaji saini wa mikataba miwili kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya **Eagle Hills Properties** ya UAE. Mikataba hiyo ni ya miradi ya uwekezaji ambapo mmoja ni wa ujenzi wa hoteli kubwa ya Nyota Tano na maeneo ya michezo katika eneo la Kizingo Maisara na wa pili ni kwa ajili ya ujenzi wa hoteli ya kisasa ya Nyota Tano na Nyumba za biashara kwa ajili ya soko la Utalii.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika mazungumzo ya Mheshimiwa Rais na Waziri wa Nchi, anaeshughulikia Mambo ya nje ya UAE Sheikh Shakhboot Al Nahyan yaliyofanyika tarehe 18 Januari, 2022. Pamoja na mambo mengine viongozi hao walizungumzia kuhusu mradi wa ujenzi wa hospitali ya Wete unaofadhiliwa na Abu Dhabi Fund kwa USD 10 Milioni. Vile vile, walizungumzia mradi wa ujenzi wa barabara ya Kisauni – Fumba pamoja na ahadi ya kutoa fedha USD 10 Milioni kwa ajili ya uwezeshaji wa vijana wajasiriamali wa Zanzibar.

31. **Mheshimiwa Spika,** Katika mazungumzo yao pia walizungumzia kuhusu ufunguzi wa Ubalozi mdogo wa UAE hapa Zanzibar na ombi la Tanzania kupatiwa kiwanja cha kujenga Ofisi na makaazi ya Balozi wa Abu dhabi. Pia walizungumzia haja ya kuangalia uwezekano wa kurudisha huduma za usafiri wa anga kwa ndege kutoka nchi za UAE hapa Zanzibar.

32. **Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo tarehe 18 Januari, 2022 Mheshimiwa Rais alikutana kwa mazungumzo ya kibiashara na uongozi wa Kampuni ya **International Holding Company (IHC)** ya Abu Dhabi ikiwa ni Kampuni kubwa ya UAE iliyoekeza katika nchi zaidi ya 30 duniani zikiwemo nchi kumi za kiafrika. Kampuni hiyo inajishughulisha zaidi na uwekezaji katika sekta ya Kilimo, Viwanda, Ujenzi, Hoteli na Usindikaji wa vyakula. Baada ya kuelezwa mipango ya Serikali ya kuendeleza Uchumi wa Buluu, Kampuni hiyo

ilionesha kuvutiwa kuwekeza Zanzibar katika sekta ya Utalii na Uvuvi.

33. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kikao cha Mheshimiwa Rais na Uongozi wa IMC, alipata fursa ya kufanya mazungumzo ya kibiashara na Kampuni ya ADQ inayomilikiwa na Serikali ya Abu Dhabi. Kampuni hiyo inajishughulisha zaidi na masuala ya Bandari, Viwanja vya ndege, Ujenzi wa barabara na vituo vya kimataifa vya mikutano. Kufuatia uwasilishaji wa fursa za uwekezaji zilizopo Zanzibar katika sekta hizo, Katibu Mtendaji wa ADQ alivutiwa zaidi na miradi ya bandari na ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano. Vile vile, tarehe 19 Januari, 2022 Mheshimiwa Rais alifanya mazungumzo na Mwenyekiti wa DP World katika Banda la DP World lililokuwepo katika maonesho ya Dubai Expo 2020.

34. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mambo mengine, viongozi hao walizungumzia azma ya DP World kuja kuwekeza Tanzania kwenye bandari ya Dar es Salaam kwa kujenga bandari ya kisasa itakayokuwa na sehemu ya kupakia na kushusha mizigo na sehemu ya mafuta na eneo huru la kiuchumi. Mheshimiwa Rais alitumia fursa hiyo kueleza Uongozi wa DP World kuwa Zanzibar ina mpango mkakati wa kujenga bandari jumuishi ya Mangapwani.

35. **Mheshimiwa Spika,** Katika maonesho ya **Dubai Expo 2020** vile vile, Mheshimiwa Rais alifanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Kampuni ya

Mafuta ya Serikali ya Dubai, ambapo Kampuni hiyo imekaribishwa kuja Zanzibar kuwekeza kwenye sekta ya bandari ya mafuta ambapo waliahidi kuanza biashara ya mafuta ya ndege wakati wakiendelea kufanya utafiti wa kuwa na bandari ya mafuta nchini.

36. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kushiriki ufunguzi wa mkutano wa **Abu Dhabi Sustainability week,** Mheshimiwa Rais alitembelea banda la Tanzania katika maonesho hayo ambapo aliwapongeza watumishi wa Tanzania kwa maandalizi na ushiriki wao. Aliridhishwa na hatua hiyo ambayo alisema inatoa nafasi ya kuitangaza Tanzania na fursa ilizonazo za uwekezaji katika Utalii, Madini, Kilimo, Nishati pamoja na uendelezaji wa Uchumi wa Buluu.

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla ziara aliyoifanya nje ya nchi Mheshimiwa Rais katika falme za Kiarabu imekua na mafanikio sana kutokana na kupata fursa ya kukutana na wadau muhimu katika utekelezaji wa mipango mikuu ya kiuchumi, hasa inayohusiana na utekelezaji na uendelezaji wa dhana ya Uchumi wa Buluu. Ziara hiyo pia imewezesha kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Zanzibar na Falme za Kiarabu (UAE) kwa faida ya Serikali na Wananchi wa pande zote mbili.

38. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio mengine ni pamoja na kuendelea kushajihisha viongozi wa Serikali na Taasisi kushiriki katika kipindi cha mahojiano

cha **'Unatekelezaje'** kinachotayarishwa na Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu. Kupitia kipindi hiki viongozi na watendaji hupata nafasi ya kueleza utekelezaji wa kazi za maendeleo ya Taasisi zao kwa kuzingatia ahadi na maagizo ya Mheshimiwa Rais sambamba na mipango ya Serikali. **'Unatekelezaje'** ni kipindi cha dakika 45, kinachorushwa hewani kupitia ZBC TV kila siku ya Jumapili saa 3:15 usiku, na ZBC Redio kila siku ya Jumatano saa 3:15 usiku. Vile vile, Zanzibar Cable TV kila siku ya Alhamis saa 3:00 usiku na marejeo ni kila siku ya Ijumaa saa 4:00 asubuhi. **Orodha ya vipindi vilivyotayarishwa inaonekana katika kiambatisho Nam. 02**

39. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeweza kutoa taarifa za matukio ya kila siku ya Mheshimiwa Rais kupitia tovuti ya Ikulu www.ikuluzanzibar.go.tz na mitandao ya kijamii ya Ikulu ya Facebook, Instagram, Twitter na Youtube kwa jina la 'Ikulu_Habari'. **Taarifa za kina kuhusu matukio hayo zinaonekana katika Kiambatisho Nam. 03 na 04.**

40. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Afisi imeongeza wigo kwa kushirikisha vyombo vya habari vingi zaidi vya ndani na nje ya nchi katika kutoa taarifa za Mheshimiwa Rais kwa jamii. Hali hii imepelekea matukio mengi ya Mheshimiwa Rais kutangazwa mbashara (live). Tunawashukuru sana wadau wetu wa habari kwa mashirikiano yao ya karibu na kuhakikisha wananchi wanapata taarifa za uhakika kwa haraka zaidi na kwa wakati.

41. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyengine Afisi inaendelea kuratibu na kusimamia utaratibu ulioanzishwa na Mheshimiwa Rais wa kuzungumza na wamiliki, wahariri na waandishi wa habari wa vyombo vya habari vya Zanzibar na Tanzania Bara kuelezea utekelezaji wa mipango ya Serikali katika kufikia malengo iliyojiwekea. Mkutano huu maalum hufanyika Ikulu kila mwisho wa mwezi. Hadi kufikia Machi 2022 jumla ya mikutano mitatu ya Mheshimiwa Rais na wadau wa habari imefanyika.

42. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Afisi imechapisha kalenda ya Ikulu nakala 4,200 inayoonesha matukio mbalimbali ya shughuli za Mheshimiwa Rais. Nakala hizo zimegaiwa katika Taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi. Aidha, kalenda hizo pia zimegaiwa kwa wananchi waliotembelea banda la maonesho ya biashara yaliyofanyika viwanja vya Maisara sambamba na kipeperushi maalumu kilichobeba taaluma ya maelekezo ya namna ya kutumia mfumo wa Sema na Rais (SNR) pamoja na baadhi ya nukuu za Mheshimiwa Rais alizotoa katika nyakati tofauti.

43. **Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa SNR umeanzishwa kwa lengo la kuwasaidia Wananchi kueleza changamoto, kero na maoni yao ili kupatiwa ufumbuzi. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Mfumo huu umepokea jumla ya malalamiko 2,817 kutoka kwa Wananchi ambapo jumla ya malalamiko 2,027 sawa na asilimia 71.95 yamepatiwa ufumbuzi na malalamiko 790 sawa asilimia 28.04 yanaendelea kufuatiliwa kwa hatua

mbali mbali ili kupatiwa ufumbuzi kupitia Taasisi zilizounganishwa kwenye mfumo huo. **Takwimu za Malalamiko yaliyowasilishwa na Wananchi katika Mfumo wa Sema na Rais kwa Kipindi cha Julai – Machi 2021/2022 zinapatikana katika kiambatisho Nam. 05 na 06.**

44. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Kitengo cha SNR kwa kushirikiana na Afisi ya Usalama wa Serikali, kimewapatia mafunzo Maafisa 90 kutoka Taasisi za Serikali zilizounganishwa na mfumo wa Sema na Rais. Mafunzo hayo yalihusu Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali, Uzalendo, Miongozo inayosimamia Usalama na Sheria zinazosimamia Usalama wa Serikali na Uhifadhi wa Nyaraka za Serikali. Vile vile Kitengo kimetoa Elimu ya matumizi ya mfumo wa Sema na Rais kwa wananchi kupitia Television (ZBC TV na ZCTV) na Redio mbali mbali (ZBC REDIO, BAHARI FM, COCONUT FM, ZENJ FM, SWAHIBA FM na REDIO MTEGANI).

45. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio yaliyopatikana kupitia Mfumo huu ni pamoja na Serikali kuwa karibu na Wananchi wake, wananchi kujenga imani na matumaini makubwa kwa Serikali, kuongezeka kwa uwajibikaji kwa Watumishi na kupunguza urasimu. Aidha, Taasisi za Serikali zimeweza kufanyiakazi hoja zinazowasilishwa na wananchi kupitia Mfumo huo. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Afisi inaendelea kutoa wito kwa Watendaji wa Serikali kushughulikia hoja zinazowasilishwa ipasavyo.

### 2. Programu Kuu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi.

46. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 801.7 Milioni kwa matumizi ya Kazi za Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 programu hii iliingiziwa jumla ya TZS. 187.6 Milioni sawa na asilimia 23 kwa matumizi ya Kazi za Kawaida.

47. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hii umeiwezesha Zanzibar kunadi na kutekeleza vyema sera ya diplomasia ya uchumi na kuendelea kuimarisha mahusiano mema yenye tija kutokana na ushiriki wake katika mikutano ya Jumuiya za Mtangamano wa Kikanda za EAC, SADC, Utatu wa COMESA - EAC- SADC, IORA, na AU - AfCFTA. Kadhalika, ushiriki katika Mikutano ya Tume za Kudumu za Pamoja (JPC) umeiwezesha Zanzibar kuimarisha mahusiano ya kindugu, kirafiki na kibiashara. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendeleza dhamira yake ya kuwahamasisha na kuwashirikisha Diaspora ili kuhakikisha wanachangia maendeleo ya kichumi na kijamii ya nchi yao ya asili (Zanzibar). Tija iliyopatikana katika shughuli za Mtangamano wa Kikanda, mikutano ya JPC na ushirikishwaji wa Diaspora imewezesha kutambua na kutangaza vivutio vya uwekezaji, Utalii, biashara na shughuli za uchumi wa buluu ndani na nje ya nchi.

48. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu ya Mtangamano wa kikanda, Zanzibar imeweza kushiriki mikutano ya Kisera na kitaalam ambayo imetoa miongozo mbali mbali ya utekelezaji mipango ya Jumuiya za Kikanda pamoja na kuandaa mikakati ya utekelezaji katika kila eneo la kisekta.

49. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar imeshiriki kikao cha 48 cha dharura cha Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kilichofanyika tarehe 25 Machi, 2022 kilichotoa mapendekezo kwa Wakuu wa Nchi kuzingatia Ripoti ya Kamati ya Uhakiki kuhusu Maombi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) ya Kujiunga na Jumuiya hiyo. Kikao hicho kilifuatiwa na Mkutano wa 19 wa Kilele wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya EAC uliofanyika tarehe 29 Machi, 2022 kwa njia ya mtandao na kuipitisha DRC kuwa Nchi Mwanachama wa EAC baada ya kukidhi vigezo vyote vilivyowekwa kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba wa kuanzishwa kwa EAC. Kadhalika, DRC imetia saini rasmi Mkataba wa kujiunga na EAC **(Treaty of Accession)** tarehe 08 Aprili, 2022 na kuifanya Jumuiya hiyo kuandika historia mpya ya kuwa na Nchi Wanachama saba (7). Naomba kutoa wito kwa Wazanzibari kuendelea kuchangamkia fursa za kiuchumi ikiwemo za biashara zinazopatikana nchini DRC na katika masoko mengine ya Jumuiya ya EAC ambapo ukubwa wa soko hilo kwa sasa umefikia zaidi ya watu milioni 300.

50. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako tukufu mambo mengine muhimu yalifanyiwa maamuzi na Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya EAC ambayo ni kuridhiwa kwa lugha ya Kifaransa kuwa lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo, kuifanya Jumuiya hiyo kuwa na lugha rasmi tatu (3) ikijumuisha Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa. Kadhalika, nomba kutoa wito kwa Wazanzibari kuendelea kujifunza lugha ya Kifaransa ili kuchangamkia fursa zinazotokana na matumizi ya lugha hiyo ikiwemo ajira na biashara katika nchi zinazotumia lugha hizo za DRC, Burundi na Rwanda. Pia, naomba kuendelea kutoa wito wa Serikali kwa wananchi kupitia Baraza lako Tukufu kuwa Lugha ya Kiswahili nayo imepata umaarufu mkubwa duniani. Taasisi nyingi za Kimataifa ikiwemo Umoja wa Afrika (AU) na Nchi mbali mbali duniani zimeanza kutambua ladha na umuhimu wa lugha ya Kiswahili kutumika katika shughuli mbali mbali za kiuchumi na maendeleo. Hivyo, nawaomba wananchi waendelee kuchangamkia fursa hizi adhim.

51. **Mheshimiwa Spika,** Afisi kwa kushirikiana na Sekta husika iliratibu ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Maonesho ya Wajasiriamali wa Nchi Wanachama ya Jumuiya ya EAC yanayojulikana kama Jua Kali/Nguvu kazi yaliofanyika tarehe 12 hadi 22 Disemba, 2021 Jijini Mwanza. Katika maonesho hayo wajasiriamali wa Zanzibar waliweza kutangaza bidhaa zao, kuuza na kutengeneza mtandao wa biashara na

masoko kwa kubadilishana taarifa mbali mbali na Wajasiriamali wa Nchi nyengine Wanachama wa EAC. Zanzibar imeendelea kutangaza bidhaa zake hasa za viungo (spices) na kupata masoko endelevu kupitia maonesho hayo. Jumla ya Wajasiriamali 52 wameweza kushiriki katika maonesho hayo muhimu ambayo hufanyika kila mwaka katika nchi wanachama kwa mzunguko. Maonesho ya mwaka 2021 yalifunguliwa na Waziri wa Biashara na Viwanda kwa niaba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufungwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Zanzibar kwa niaba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Naomba kuwahakikishia kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendeleza azma yake ya kuwatengenezea wajasiriamali na wafanyabishara mazingira bora ya kufanya shughuli zao ikiwemo kupata masoko ya uhakika na endelevu.

52. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuendelea kutafuta masoko kwa ajili ya wafanyabiashara na wajasiriamali, Serikali kwa kushirikiana na sekta husika iliratibu kufanyika kwa Maonyesho ya Kitaifa ya Biashara ya bidhaa za Viwanda sambamba na Kongamano la Uwekezaji katika kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyofanyika kuanzia tarehe 3 hadi 9 Disemba, 2021 Zanzibar. Lengo la Kongamano la Uwekezaji ni kutangaza fursa mbali mbali za Uwekezaji katika Sekta ya Uchumi wa Buluu, Utalii, Afya, Madini, Viwanda na Miundombinu ya

Uchukuzi. Kongamano la Uwekezaji lilifunguliwa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kongamano hilo lilihudhuriwa na zaidi ya wawekezaji 300 kutoka nchi mbali mbali zikiwemo Misri, India, Afrika Kusini, China na Umoja wa Falme za Kiarabu.

53. **Mheshimiwa Spika,** ipo mikutano ya Kisekta na kitaalamu iliyofanyika katika kipindi hiki cha bajeti inayoishia Juni, 2022 ikiwemo mikutano ya Kamati ya Kitaifa inayoratibu, kusimamia na kuondosha Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiforodha **(Non-Tariff Barriers - NTBs)** ambayo kwa upande wa Tanzania ilifanyika Tanzania bara na Zanzibar. Mfumo wa kufuatilia na kuripoti NTB's uliimarishwa, marekebisho ya Sheria ya NTB's ya mwaka 2017 **(NTB's Act 2017)** yamefanyika na jumla ya vikwazo 230 vimepatiwa ufumbuzi toka kuanza kwa vikao vya aina hii mwaka 2010. Hivyo, EAC inaendelea kuimarika na kuwa ukanda salama bila ya vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiforodha.

54. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja imefanya marekebisho ya Sheria, kanuni na miongozo ambayo haiendani na utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki **(Technical Support to the Amendment Law, Regulations, and Guidelines Inconsistent with the EAC Common Market Protocol).** Kadhalika, utekelezaji wa Ibara ya 24 ya Sheria

ya Umoja wa Forodha wa EAC 2004 inayotia nguvu kuanzishwa kwa Kamati ya pamoja ya EAC ya kutatua migogoro ya biashara **(Trade remedies committee)** imefikia hatua nzuri na kutoa mapendekezo ya kuharakishwa uundaji wa kamati hiyo baada ya mazingatio maalum ikiwemo kuhusisha wajumbe kutoka nchi nyengine Wanachama zilizojiunga na Jumuiya, kutofautisha kazi na mamlaka ya Kamati hii na Kamati nyengine ikiwemo kamati ya NTBs. Lengo la kuundwa Kamati hii ni kuharakisha upatikanaji wa suluhu za kudumu na zenye nguvu ya kisheria ya migogoro ya biashara katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya EAC. Katika kipindi cha miezi sita Julai hadi Disemba, Zanzibar iliripoti kwenye Kamati hiyo utoaji vibali vya kazi na ukaazi 16 katika kuimarisha mzunguko huru wa watu na wafanyakazi **(Free Movement of People and Labour)** kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vibali hivyo vimetolewa katika eneo la utoaji wa huduma mbali mbali ikiwemo sekta ya utalii.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Eneo Huru la Biashara la Afrika lililoanza rasmi mwezi Januari, 2021, SMZ kwa kushirikiana na SMT iliratibu mafunzo maalum yaliyowakutanisha wataalam kutoka Taasisi za Umma na binafsi yaliofanyika kuanzia tarehe 13 hadi 15 Disemba, 2021 Zanzibar. Mafunzo hayo yaliwashirikisha wadau kutoka Taasisi zinazoshughulikia masuala ya Biashara, Forodha, Wajasiriamali, Fedha, Uingizaji na Usafirishaji wa mizigo. Lengo la mafunzo hayo

ni kuwajengea uwezo Wataalam wetu ili kumudu ushindani katika soko hilo kubwa la Afrika pamoja na kujipanga kimkakati katika kuchangamkia fursa za Soko la AfCFTA. Kadhalika, kuongeza kasi ya utekelezaji wa maagizo ya Wakuu wa Nchi katika kuelekea Uchumi Mmoja wa Afrika **(Economic Union of Africa).** Hatua inayoendelea katika majadiliano yanayowahusisha Nchi wanachama katika Soko la AfCFTA ni kukamilisha majadiliano ya Uasili wa Bidhaa ili kuwa rahisi kuzitambua bidhaa zinazozalishwa ndani ya bara la Afrika ambazo ndizo zinazohusika na fursa za soko hilo.

56. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu iliunda Kamati Maalum kwa ajili ya kufuatilia malalamiko ya wavuvi na wafanyabiashara wa Wilaya ya Micheweni Pemba. Malalamiko hayo yanahusu changamoto wanazokumbana nazo wakiwa katika shughuli za kiuchumi na kijamii Jijini Mombasa, Kenya. Hii imetokana na malalamiko waliyoyatoa wananachi wa Micheweni wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoifanya Pemba tarehe 31 Agosti, 2021. Wananchi hao kihistoria wamekuwa wakishirikiana kwa karibu katika mambo mbali mbali ya maendeleo na wananchi wa Kaunti za Mombasa, Kilifi, Lamu, Kwale, Tana River na Taita Taveta.

57. **Mheshimiwa Spika,** Kamati tayari imewasilisha taarifa yake Serikalini yenye mapendekezo ikiwemo kuwasilisha baadhi ya changamoto hizo katika Tume ya Pamoja ya Ushirikiano baina

ya Tanzania na Kenya **(Joint Commission for Cooperation - JCC).**

58. **Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ilifanya mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali tarehe 17 hadi 18 Agosti, 2021 Jijini Lilongwe, Malawi. Katika mkutano huo, Ujumbe wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tanzania ilikubali dhamana ya kuwa mwenyeji wa Kituo cha kikanda cha SADC cha kupambana na Ugaidi pamoja na kukubali kubeba gharama za kituo hicho kwa kipindi cha mpito kuanzia mwaka 2021 hadi 2024. Lengo la kuanzishwa kituo hicho ni kuwa na mkakati wa pamoja wa nchi za SADC katika kukabiliana na tishio la matukio ya kigaidi ambapo kwa sasa yamekuwa yakitishia usalama wa Nchi Wanachama. Kadhalika, kitakuwa kiini cha kukusanya na kuchakata taarifa za kiintelijensia ambazo zitasaidia kubaini njia wanazotumia wenye makundi ya kigaidi. Kituo hicho kilizinduliwa rasmi tarehe 28 Februari, 2022 Jijini Dar es Salaam. Masuala mengine yaliofanyiwa maamuzi na Wakuu wa Nchi na Serikali ni kuridhia mabadiliko ya Jukwaa  la Bunge la SADC kuwa Bunge la SADC la ushauri na majadiliano pamoja na kumteuwa Mheshimiwa Dk. Lazarus McCarthy Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya SADC kwa kipindi cha mwaka mmoja 2021/2022.

59. **Mheshimiwa Spika,** Afisi iliratibu na kushiriki Mkutano wa Baraza la Mawaziri uliofanyika tarehe 18 hadi 19 Machi, 2022 Jijini Lilongwe, nchini Malawi. Mawaziri wa SADC katika mkutano huo walipitisha bajeti ya SADC 2022/2023 ambayo pamoja na masuala mengine, hutumika kutekeleza miradi ya Jumuiya. Miongoni mwa miradi itakayonufaika na bajeti hiyo ni kutafsiri nyaraka muhimu mbali mbali za kisheria na kisera kwa lugha ya Kiswahili ambapo jumla ya USD 73,518 zilidhinishwa. Mradi mwengine utakaonufaika na bajeti hiyo ni mradi wa kutafsiri Machapisho ya Brigedia Jenerali Mstaafu Hashim Mbita ambapo jumla ya USD 359,503 zitahitajika ili kukamilisha agizo la kutafsiri vitabu tisa vinavyohusu mradi huo kwa Lugha ya Kiswahili.

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa shughuli za Jumuiya ya Nchi zilizopo katika mwambao wa Bahari ya Hindi **(Indian Ocean Rim Association - IORA),** Afisi iliratibu ushiriki wa Mkutano wa 11 wa Kamati ya Makatibu Wakuu wa Jumuiya hiyo uliofanyika Jijini Dar es Salaam pamoja na Mkutano uliofanyika mwezi Septemba, 2021. Masuala mbali mbali ya kimkakati yalijadiliwa ili kufikia maendeleo endelevu ya shughuli za kiuchumi na miundombinu katika Nchi Wanachama wa IORA ikiwemo mkakati wa vigezo vya ushirikishwaji wa washirika wa mazungumzo, mpango kazi wa Jumuiya ya IORA, vigezo vya kuomba uwanachama wa Jumuiya ya IORA na masuala ya ulinzi na usalama wa bahari ya Hindi.

61. **Mheshimiwa Spika,** Masuala mengine yaliyojadiliwa ni Ushirikiano katika biashara na uwekezaji, Uimarishaji wa uvuvi endelevu wa bahari ya Hindi, Menejimenti ya kukabiliana na maafa, Elimu, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu, Utalii na Utamaduni, Uchumi wa Buluu, Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na Kuimarisha Mashirikiano Baina ya Taasisi za Umma na Binafsi.

62. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwakumbusha Wajumbe kuwa lengo kuu la Mheshimiwa Rais la kuweka kipaumbele suala la Uchumi wa Buluu katika Serikali anayoiongoza linatokana na kuongezeka kwa uelewa wa Jumuiya za Kimataifa na za Kikanda duniani kuhusu shughuli za kiuchumi zinazotokana na Bahari kuwa ni mkombozi wa maendeleo ya binaadamu. Kadhalika, suala la uchumi wa bahari pamoja na kuungwa mkono na Jumuiya ya IORA, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 kupitia Ibara ya 136 (e) imelieleza na kulipangia mikakati ya Utekelezaji. Natumia nafasi hii kuliomba Baraza lako Tukufu liendelee kuwahamasisha Wananchi wachangamkie kikamilifu fursa zinazotokana na Uchumi wa Buluu.

63. **Mheshimiwa Spika,** ili Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia lengo na shabaha ya IORA, Wataalamu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar walikutana kuanzia tarehe 13 hadi 16 Septemba 2021 Zanzibar kuandaa mkakati wa pamoja ambao pamoja na mambo mengine,

unalenga kuimarisha vikundi kazi ambavyo vitasaidia utekelezaji wa programu mbali mbali katika mtangamano huo.

64. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilishiriki katika Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya uliyofanyika tarehe 9 hadi 12 Machi, 2022 Zanzibar. Mkutano huo ulijadili kuimarisha ushirikiano na mashauriano katika maeneo ya Diplomasia, Ulinzi na Usalama, Miundombinu, uchumi na masuala ya kijamii. Vile vile, Mkutano ulifanikiwa kuondoa vikwazo 10 vya biashara visivyokuwa vya kiforodha na kufanya jumla ya vikwazo 56 kuondoshwa tangu kuanza mikutano hii mwaka 2017 kwenye maeneo mbali mbali ikiwemo biashara haramu ya madini, upatikanaji wa vibali vya kazi, tozo za matumizi ya barabara pamoja na changamoto zinazojitokeza katika maeneo ya mipakani.

65. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Serikali imeshiriki katika Mkutano wa Tume ya Kudumu ya Pamoja baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu uliofanyika kuanzia tarehe 13 hadi 14 Aprili, 2022 Jijini Dar es Salaam. Masuala muhimu ya ushirikiano yaliyojadiliwa ni pamoja na Uchumi, Uwekezaji, Elimu, Ajira, Utalii, Muindombinu, Nishati, Madini, Kilimo, Uvuvi, Uchumi wa Buluu, Ulinzi na Usalama. Kwa upande wa Zanzibar, Miradi iliyopendekezwa kuweza kunufaika na mashirikiano hayo ni

Ujenzi wa bandari ya makontena na mizigo mikubwa pamoja na gati ya mafuta na gesi huko Mangapwani, ujenzi wa kituo cha meli (Cruise), ujenzi wa kituo cha abiria cha ndani katika Bandari ya Malindi, ujenzi wa bandari ya mizigo na abiria ya Wete Pemba na ujenzi wa bandari ya mizigo na abiria ya Kizimkazi.

66. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutambua umuhimu wa kushirikiana na Wanadiaspora katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yao ya asili. Aidha, Wanadiaspora wanaendelea kuitikia wito wa Serikali kwa kuwekeza katika maeneo mbali mbali, kuwa mabalozi wa kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji na kuchangia katika maendeleo ya kijamii hususan sekta ya Afya, Elimu na watu wenye uhitaji maalum. Kwa kuthamini mwitikio huo wa wanadiaspora, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi zote ambazo Diaspora hushirikiana nazo ikiwemo Idara ya Uhamiaji, Kamisheni ya Kazi, Bodi za Mapato na Taasisi za Usajili zipo katika hatua za mwisho kuandaa muongozo wa kuwapa Hadhi Maalum Wanadiapora. Serikali zote mbili zimeanza kuwasajili wanadiaspora kupitia data base na kuweka madeski maalum ya kisekta ili kurahisisha upatikanaji wa huduma wanazozihitaji ikiwemo kuanza matayarisho ya awali ya kutoa vitambulisho vya Wanadiaspora. Baada ya kukamilika kwa muongozo wa Hadhi Maalum, Serikali italiarifu Baraza lako tukufu na

kutoa uelewa kwa jamii na hasa wanadiaspora namna ya kupata huduma hizo.

67. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako kuwa, Ujumbe wa wanadiaspora kutoka Marekani **(Tanzania Diaspora HUB)** ulifanya ziara Zanzibar kuanzia tarehe 31 Disemba, 2021 hadi 5 Januari, 2022 na kupata fursa kujionea na kuelewa fursa za uwekezaji, vivutio vya utalii na maeneo ya kuchangia katika huduma za kijamii. Kwa upande wa Unguja, Wanadiaspora walitembelea maeneo ya shamba la viungo Kizimbani na Mabwawa ya samaki na Kasa ya UWEMAJO Jozani. Kwa upande wa Pemba, Ujumbe huo ulitembelea Kisiwa cha Misali, Mabwawa ya Samaki yaliopo Pujini, maeneo tengefu ya uchumi ya Chamanangwe na Micheweni na maeneo ya vivutio vya utalii ya Vumawimbi na Makangale. Aidha, Ujumbe wa Wanadiaspora ulitembelea maeneo mbali mbali na kutoa vifaa katika kituo cha watoto yatima kilichopo Micheweni.

### 3. Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Afisi ya Rais Ikulu.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 1,111.0 Milioni kwa matumizi ya Kazi za Kawaida na TZS. 6,000.0 Milioni kwa Mradi wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 programu hii iliingiziwa jumla ya TZS. 241.8 Milioni sawa na asilimia 21 kwa matumizi ya Kazi za Kawaida. Kwa upande wa Mradi wa Maendeleo fedha zilizoingizwa ni TZS. 500 Milioni.

69. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii umepelekea Afisi ya Rais Ikulu kupata mafanikio makubwa katika kuimarisha mazingira ya utumishi kwa kuwapatia watumishi stahiki zao na vifaa vya kufanyia kazi ikiwemo gari na vyombo vya moto vya maringi mawili.

70. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao ikiwemo mishahara, posho za likizo, posho la kukaimu, malipo baada ya saa za kazi na stahiki nyenginezo kwa mujibu wa sheria. Aidha, imeimarisha mazingira ya Afisi pamoja na uendeshaji. Vile vile, imefanikiwa kuratibu na kusimamia vikao vinne vya Bodi ya Zabuni. Vikao hivi vilijadili na kupendekeza njia mbadala ya kuweza kutatua changamoto za upatikanaji wa bidhaa na huduma. Kupitia mapendekezo yaliyotolewa na Bodi ya Zabuni tayari imeshafanya makubaliano na wasambazaji wa bidhaa na watoa huduma kulingana na mahitaji ya Afisi. Aidha, kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na nidhamu kazini, Afisi inaendelea kuimarisha mfumo wa usajili wa kuingia na kutoka kazini **(Biometric Registration System)** pamoja na kuhimiza uvaaji wa mavazi yenye staha kwa watumishi na wageni wanaofika Afisi ya Rais Ikulu.

71. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanikiwa kuibua maeneo ya kimkakati ya kuandikia miradi, ambapo maandiko ya awali ya dhana ya miradi sita **(Concept Note)** tayari yametayarishwa. Maandiko hayo yanajumuisha Mradi wa Ukarabati

wa Nyumba za Ikulu na nyumba za Viongozi, Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais, Mradi wa Mageuzi ya Kidijitali na Kuijengea uwezo Afisi ya Rais Ikulu na Mradi wa Kudhibiti Mmong'onyoko wa ardhi katika Ikulu ndogo Bwefum na Mkokotoni.

72. **Mheshimiwa Spika,** Mengine ni Mradi wa uanzishaji wa Mfumo wa Kidijitali wa Usajili wa Wanadiaspora wa Zanzibar pamoja na Mradi wa Ukarabati na kujenga uwezo kwa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar. Katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za miradi hiyo, Afisi inapanga kutumia njia mbali mbali za kuitekeleza. Aidha, Afisi inaendelea kuandaa Mpango Mkakati ili kwenda sambamba na mageuzi yaliyofanyika hivi karibuni. Utayarishaji wa Mkakati huo unazingatia kikamilifu Miongozo Mikuu ya Kitaifa.

73. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Usalama wa Serikali Zanzibar imefanikiwa kuwafanyia upekuzi wa kiusalama watumishi 314 kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali na sekta binafsi waliopo Unguja na Pemba. Kati ya hao 14 walifanyiwa upekuzi wa awali kwa kibali maalum, 14 walifanyiwa upekuzi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo **(Security Clearency),** 229 walifanyiwa upekezi maalum na 57 walifanyiwa upekuzi endelevu. Sambamba na hayo, Afisi ilifanya semina juu ya utunzaji wa Nyaraka na uhifadhi wa Siri za Serikali ambapo jumla ya watumishi 500 kutoka Taasisi za

Serikali wameshiriki. **Ufafanuzi wa Watumishi waliopatiwa Semina ya Utunzaji Nyaraka na Udhibiti wa Siri za Serikali unapatikana katika kiambatisho Nam. 07.** Kufanyika kwa semina kumesaidia kuleta mabadiliko katika utunzaji wa Nyaraka na Kumbukumbu za Serikali pamoja na kuimarika kwa utendaji wa masjala katika Afisi za Serikali na urekebishaji wa kasoro katika majengo ya Serikali yaliyokaguliwa. Aidha, ukaguzi wa kiusalama katika majengo ya Serikali umefanyika ambapo Taasisi zilizokaguliwa zilipewa ushauri wa kiusalama ili kuondoa changamoto zilizobainika. Matokeo ya ukaguzi huo, yalipelekea watumishi kufanyakazi katika mazingira salama kutokana na kufanyiwa kazi mapendekezo yaliotolewa kila baada ya ukaguzi kukamilika.

74. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu - Pemba imeendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa ufanisi ikiwemo kuhudumia na kuziweka salama nyumba za Ikulu zilizopo Pemba. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Afisi imefanikiwa kuimarisha nyumba ya Ikulu ya Pagali na Mkoani kwa kufanya matengenezo madogo madogo ikiwemo matengenezo ya jenereta 2. Aidha, Afisi imefanikiwa kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Mtumishi mmoja anaendelea na mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza katika masuala ya fedha na watumishi 43 wamepatiwa mafunzo ya ndani juu ya maadili, haki na fursa kazini.

## 4. Programu Kuu ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka.

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii, ilitarajiwa kukusanya mapato ya TZS. 15.0 Milioni. Hadi kufikia Machi, 2022 ilikusanya TZS. 2.9 Milioni ambazo ni sawa na asilimia 19.3.

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 574.9 Milioni kwa matumizi ya Kazi za Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 programu hii iliingiziwa jumla ya TZS. 318.4 Milioni sawa na asilimia 55 kwa matumizi ya Kazi za Kawaida.

77. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanya ukaguzi wa kumbukumbu na nyaraka kwa Wizara sita (6) pamoja na Taasisi zake sambamba na kutoa elimu juu ya namna bora ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu. Aidha, imewahudumia Watafiti 818 wa ndani na Watafiti sita (6) kutoka nje ya nchi. Vile vile, Afisi imetangaza na kutoa taalauma kuhusu kazi, majukumu na umuhimu wa nyaraka zinazohifadhiwa na Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar kupitia Maonesho ya Biashara ya kuadhimisha Miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Afisi pia, imefanya ukarabati wa baadhi ya sehemu za jengo la Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu, kuwajengea uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watumishi 27 wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar.

78. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea na shughuli za uhifadhi na usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu Pemba, ikiwa ni pamoja na kujenga mashubaka (shelves) na kuhamisha nyaraka kutoka jengo la makumbusho liliopo Hospitali ya Chake Chake na kuhamishiwa katika jengo la Afisi ya Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu.

## MAFANIKIO YA FUNGU A02

### 5. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi fungu A02 lilitengewa jumla ya TZS 2,194.5 Milioni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 fungu hili liliingiziwa TZS 1,181.8 Milioni ambazo ni sawa na asilimia 53 ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka. Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu za Fungu hili ni kama ifuatavyo:-

80. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni pamoja na kuimarika Sheria, Sera na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo ya nchi na kudumisha amani na mshikamano nchini. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii iliidhinishiwa TZS 687.2 Milioni.

81. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kufanikisha vikao vya kawaida na dharura vya

Baraza la Mapinduzi na Kamati zake ikiwemo Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu ambapo pamoja na mambo mengine, nyaraka mbali mbali zikiwemo za Sera na Sheria ziliwasilishwa, kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

**82. Mheshimiwa Spika,** mbali ya mafanikio hayo, katika kipindi hiki, Afisi imesimamia uapishwaji wa viongozi wa Serikali waliochanguliwa kushika nyadhifa mbali mbali katika Taasisi za Umma. Aidha, Serikali kupitia Afisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kushirikiana na Taasisi ya UONGOZI ya Dar es Salaam iliandaa mafunzo kwa Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wengine waandamizi kuhusu Uandishi wa Sera. Mafanikio mengi yamepatikana kutokana na mafunzo hayo ikiwemo kuongezeka uelewa wa watendaji wa ngazi za juu katika kuibua vipaumbele vya Sera na uandishi wake.

**83. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika Programu hii, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa katika kipindi hiki Afisi pia imekamilisha Ripoti ya Tathmini ya Fursa za Ajira kwa Vijana katika Sekta Binafsi Zanzibar na Ripoti ya Tathmini ya Hali ya Rushwa katika Sekta za Utoaji Huduma za Umma, Zanzibar. Kuandaliwa kwa Ripoti hizi kunatokana na dhamira ya Serikali kuyawezesha makundi mbali mbali katika jamii wakiwemo vijana pamoja na kuhakikisha Taasisi za Umma zinazingatia kikamilifu misingi ya Utawala Bora katika utoaji wa huduma.

## 6. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

84. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Afisi, uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu muhimu, mazingira ya kazi, kuongeza ufanisi na uwajibikaji kazini. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu hii iliidhinishiwa TZS 1,507.3 Milioni.

85. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyofikiwa kutokana na utekelezaji wa Programu hii ni pamoja na kuimarika mazingira ya kazi na kuipatia Afisi vifaa stahiki kwa ajili ya utunzaji Kumbukumbu. Kadhalika, uwezo wa watumishi wetu umeendelea kuimarika na kuwa wenye ufanisi zaidi kutokana na kuendeleza programu za kujenga uwezo wao kitaaluma kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kulingana na mahitaji na mabadiliko ya wakati. Hadi hivi sasa, watumishi wanne wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Stashahada katika fani ya Rasilimali Watu na Shahada ya Kwanza katika fani za Utunzaji Kumbukumbu na Ununuzi na Ugavi. Watumishi wengine sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika masuala ya Itifaki, Usimamizi wa Fedha, Udereva wa Viongozi Mashuhuri. Aidha, Afisi imewapatia watumishi wake taaluma ya namna ya kujikinga na maradhi yasiyoambukiza na Uviko 19.

## MWELEKEO WA BAJETI YA AFISI YA RAIS IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

86. **Mheshimiwa Spika,** hotuba ya bajeti ya Afisi ya Rais Ikulu ya mwaka wa fedha 2022/2023 ni ya kwanza katika muhula wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nane, baada ya Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzisha Afisi ya Rais Ikulu mnamo tarehe 10 Julai, 2021. Hotuba hii imezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo **Zanzibar Developement Plan - ZADEP,** Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mipango Endelevu ya Milenia **(SDGs)** na Maelekezo na Miongozo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

87. **Mheshimiwa Spika,** naomba kulihakikishia Baraza lako kuwa, Afisi ya Rais Ikulu itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo na miongozo madhubuti ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane imeiandaa. Lengo ni kuhakikisha Afisi inatoa mchango mkubwa na kuhakikisha kuwa Zanzibar inapiga hatua zaidi za kimaendeleo pamoja na kudumisha mafanikio yaliopatikana.

88. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-
    i. Kuratibu na kusimamia shughuli na huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,

ii. Kusimamia majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake,
iii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za Wizara, Idara na Taasisi za Serikali pamoja na maamuzi ya Serikali,
iv. Kuwawezesha wananchi kupata taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali yao,
v. Kuratibu ushiriki wa watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mtangamano wa Jumuiya za Kikanda yenye kuleta tija.
vi. Kuwashajihisha Wanadiaspora kuchangia katika maendeleo ya Zanzibar,
vii. Kuimarisha mazingira na usalama katika nyumba za Ikulu, Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma,
viii. Kuimarisha shughuli za uhifadhi wa Nyaraka na kumbukumbu Zanzibar,
ix. Kuimarisha usalama kwa watumishi wa Serikali na maeneo wanayofanyia kazi; na
x. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuipatia Afisi vitendeakazi kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu.

## PROGRAMU KUU NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA ZINAZOHITAJIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

89. **Mheshimiwa Spika,** Programu, viapumbele na shughuli za Afisi ya Rais Ikulu zitatekelezwa na Afisi na Idara zifuatazo:-
i. Afisi ya Faragha ya Rais;
ii. Afisi ya Baraza la Mapinduzi;

iii. Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu;
iv. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi;
v. Idara ya Utumishi na Uendeshaji;
vi. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
vii. Taasisi ya Nyaraka na kumbukumbu Zanzibar;
viii. Afisi ya Usalama wa Serikali; na
ix. Afisi ya Rais Ikulu – Pemba.

90. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu Fungu A01 ina jumla ya Programu Kuu nne (4) na Programu Ndogo kumi (10) kama ifuatavyo:-

**1. Programu Kuu ya Kusimamia na Kuratibu Shughuli na Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu.**

91. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuratibu na kusimamia huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais na kuimarisha mawasiliano baina ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wananchi wake. Aidha, kuendeleza Taswira nzuri ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni Umma na Wananchi wote kwa jumla kuwa na uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo tatu zifuatazo:-
i. Programu Ndogo ya Kusimamia huduma na shughuli za Mheshimiwa Rais,
ii. Programu Ndogo ya Kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi, na

iii. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miradi ya Kimkakati ya Serikali.

92. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kufuatilia maagizo na maelekezo yanayotokana na shughuli za Mheshimiwa Rais;
ii. Kupanga na kutekeleza mahitaji ya Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kutekeleza kazi zake;
iii. Kuimarisha huduma kwa kuzipatia vifaa na bidhaa nyumba za Ikulu zilizopo Unguja, Pemba, Dar – es - Salaam na Dodoma;
iv. Kuifanyia matengenezo nyumba ya Ikulu ya Mnazi Mmoja na Ikulu ndogo zilizopo Dar – es - Salaam, Unguja, Dodoma na Pemba;
v. Kuimarisha maktaba ya Mheshimwa Rais,
vi. Kuandaa mikutano ya Mheshimiwa Rais na makundi mbali mbali ya kijamii;
vii. Kuimarisha mfumo wa mawasiliano wa Sema na Rais (SNR);
viii. Kuimarisha mawasiliano kupitia Mitandao ya Kijamii na kutathmini matumizi ya TEHAMA katika Afisi ya Rais Ikulu;
ix. Kukuza mawasiliano baina ya Ikulu, Wananchi na Wadau wa habari, na
x. Kufuatilia Miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na Taasisi za Serikali.

93. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Kuratibu na Kusimamia Shughuli na Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TZS. 5,908.4 Milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika programu hii.

**2. Programu Kuu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi.**

94. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha mashirikiano na Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi katika maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya Zanzibar. Aidha, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni Zanzibar kufaidika na fursa za Kiuchumi na Kijamii zinazotokana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kikanda na Kimataifa, na
ii. Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi.

95. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-
   i. Kuratibu na kushiriki katika mikutano ya kikanda ndani na Nje ya Nchi;
   ii. Kuendeleza ushirikiano wa kimataifa;
   iii. Kujenga uelewa kwa jamii juu ya Sera ya Diaspora ya Zanzibar na utekelezaji wake;
   iv. Kujenga uelewa juu ya fursa zinazopatikana kutokana na Jumuiya za Mtangamano wa Kikanda (EAC, SADC, IORA, TRIPATITE na AU); na
   v. Kushiriki katika mikutano ya ndani na kimataifa inayohusiana na Diaspora.

96. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TZS. 929.2 Milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika programu hii.

### 3. Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Afisi ya Rais Ikulu.

97. **Mheshimiwa Spika,** malengo makuu ya Programu hii ni kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kuratibu shughuli za Afisi ya Rais Ikulu; Kuimarisha Shughuli za Mipango; Kuandaa na Kuchambua Sera na Kufanya Utafiti; Kuimarisha Shughuli za Upekuzi kwa Watumishi kabla na baada ya Kuajiriwa; Kuimarisha Usalama wa Majengo na Miundombinu ya Serikali pamoja na kuratibu

na kusimamia shughuli za Afisi ya Rais Ikulu - Pemba. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi pamoja na Ufuatiliaji wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo nne zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu na usimamizi wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu;
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Afisi ya Rais Ikulu;
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu - Pemba; na
iv. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama wa watumishi wa Umma.

98. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia mafanikio ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kulipa mishahara kwa wafanyakazi na stahiki zao,
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi,
iii. Kufanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali watu,
iv. Kuandaa na kuratibu mikutano ya kamati tendaji na kamati ya Uongozi ya Afisi ya Rais Ikulu,
v. Kutoa huduma za uendeshaji na Utawala katika Afisi ya Rais Ikulu,
vi. Kufanya ukaguzi wa hesabu za awali na endelevu na Vikao vya Kamati ya ukaguzi,
vii. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Afisi ya Rais ikulu,

viii. Kuandaa Mpango Mkakati wa mawasiliano kwa Afisi ya Rais ikulu,
ix. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu,
x. Kufanya Utafiti kuhusu uelewa wa jamii juu ya dhana ya Diaspora na umuhimu wake,
xi. Kufanya marekebisho ya sharia ya Diaspora Zanzibar,
xii. Kutoa huduma za uendeshaji na Utawala katika Afisi ya Rais Ikulu - Pemba;
xiii. Kufanya upekuzi wa awali wa kiusalama na endelevu kwa wafanyakazi, na
xiv. Kufanya ukaguzi wa kiusalama katika majengo na miundombinu ya Serikali.

99. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Afisi Rais Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TZS. 3,505.3 Milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika programu hii.

**4. Programu Kuu ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka.**

100. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni Kusimamia Nyaraka na Kumbukumbu zote za Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kwa Taasisi zake zilizopo Zanzibar. Programu hii ina Programu Ndogo moja ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka.

101. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-
   i. Kuhaulisha na kuhuisha nyaraka zilizochakaa,
   ii. Kufanya ukaguzi na upembuzi wa awali wa mahitaji ya mafunzo ya vitendo kwa wasimamizi wa kumbukumbu na nyaraka,
   iii. Kutayarisha Mpango Mkakati wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar,
   iv. Kuwajengea uwezo watumishi wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar, na
   v. Kufanya utambuzi wa nyaraka ziliopo kwa wananchi.

102. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka kwa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TZS. 758.6 Milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika programu hii.

103. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Baraza la Mapinduzi Fungu A02 ina jumla ya Programu Kuu mbili (2) na Programu Ndogo tatu (3) kama ifuatavyo:-

**5. Programu ya Uratibu wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi.**

104. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kuimarisha Sera, Sheria na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo na kuimarisha uwajibikaji wa watumishi wa umma.

Aidha, kuhakikisha malengo na majukumu ya Wizara na Taasisi za Serikali yanatekelezwa ipasavyo na kufikiwa kwa ufanisi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo na kudumisha amani na umoja Nchini. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo: -

i. Uratibu wa Shughuli za BLM na Majukumu ya KBLM/KMK; na
ii. Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi wa Taasisi za Umma.

105. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa: -

i. Kutayarisha vikao vya kawaida vya BLM na Kamati ya Makatibu Wakuu.
ii. Kutayarisha vikao Maalum vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake.
iii. Kufanya uchambuzi wa Nyaraka zinazowasilishwa Baraza la Mapinduzi kupitia Kamati ya Makatibu Wakuu.
iv. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya BLM na Kamati zake pamoja na masuala maalum yanayohusu Sera, Sheria na Maamuzi ya Serikali.
v. Kuandaa vikao vya kuhimiza uwajibikaji wa watumishi wa Umma kati ya KBLM/KMK na Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi za SMZ; na
vi. Kuimarisha Taswira na hali ya Utumishi wa Umma Nchini.

106. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Uratibu wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya BLM iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya TZS. 856.8 Milioni zinahitajika kwa matumizi ya shughuli zilizopangwa.

### 6. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Afisi ya Baraza la Mapinduzi.

107. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha mazingira ya kazi, kuongeza ujuzi na ufanisi wa wafanyakazi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuwa na mfumo bora wa kisasa wa kuendesha shughuli za Afisi na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu.

108. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuimarisha miundombinu ya Afisi, majengo pamoja na mazingira yake.
ii. Kuimarisha huduma za mawasiliano na utekelezaji wa kazi za kila siku za Afisi.
iii. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi wa Afisi.
iv. Kutoa taaluma ya afya kuhusu kujikinga na maradhi yasiyoambukiza na VVU/UKIMWI.

109. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Afisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya TZS. 1,577.8

Milioni zinahitajika kwa matumizi ya shughuli zilizopangwa.

## MAMBO MAKUU YATAKAYOTEKELEZWA NA AFISI YA RAIS IKULU KWA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023

**110. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu, katika utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imezingatia vipaumbe vifuatavyo:-

i. Kuimarisha mfumo wa ulinzi na usalama katika majengo ya Ikulu na makaazi ya Mheshimiwa Rais; na
ii. Kujenga Ikulu ndogo (State Lodges).

**111. Mheshimiwa Spika,** ili shughuli hizi ziweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TZS. 4,000 Milioni zinahitajika kwa matumizi ya shughuli zilizopangwa.

## MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**112. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Afisi ya Rais Ikulu kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kwa fungu A01 na A02 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Afisi ya Rais Ikulu zenye jumla ya TZS 17,536.03

Milioni. Kati ya fedha hizo, TZS 13,536.03 Milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS 4,000 Milioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maedeleo. **Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika kiambatisho Nam. 08.**

## HITIMISHO

113. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu lisiache kutushauri na kutupatia miongozo wakati wowote itakapoona kunahaja ya kufanya hivyo. Naahidi tutaufanyia kazi ushauri na miongozo yenu. Naomba kwa umoja wetu tumpatie mashirikiano makubwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ndie msimamizi mkuu wa Afisi hii. Aidha, nakuombeni Viongozi wenzangu na Wafanyakazi tufanye kazi kwa bidii na uweledi mkubwa zaidi ili tulinde mafanikio tuliyoyapata na tufikie matarajio ya wananchi kwa Nchi yetu. Naomba tuifanyie kazi kwa vitendo kauli ya Mheshimiwa Rais isemayo **"Yajayo ni neema tupu".**

114. **Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza kusoma Hotuba ya Bajeti ya Afisi ya Rais Ikulu, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu ndugu Mussa Haji Ali, Wakurugenzi na watendaji wa ngazi zote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika utendaji na usimamizi wa shughuli za kila siku. Tuombeane kheri, baraka na fanaka katika

mwezi huu mtukufu wa ramadhani (Ramadhan Kareem). Namuomba Mwenyezi Mungu, subhanahu Wa Taala, atuondoshee mitihanai ya maradhi na atuzidishie neema katika nchi yetu.

115. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Magomeni kwa mashirikiano wanayonipa katika kuwatumikia na ujenzi wa Taifa letu.

116. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili sambamba na kutupatia ushauri na maelekezo ambayo yataimarisha utekelezaji na hatimae liipitishe bajeti hii.

117. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Ahsanteni.

……………………………………………..
Jamal Kassim Ali
Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais – Ikulu

**Kiambatisho Nam. 1. Mchanganuo wa Maagizo kwa kila Mkoa**

| Nam. | Jina la Mkoa | Idadi ya Maagizo | Maagizo yaliyotekelezwa | Asilimia ya maagizo yaliyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kaskazini Unguja 05 na 6 Julai, 2021 | 12 | 9 | 75.0 |
| 2 | Kusini Unguja 03 na 4 Julai 2021 | 10 | 10 | 100.0 |
| 3 | Mjini Magharibi 03 Julai, 2021 | 8 | 8 | 100.0 |
| 4 | Kaskazini Pemba 30 Agost hadi 01 September 2021 | 16 | 14 | 87.5 |
| 5 | Kusini Pemba 02 na 03 Julai 2021 | 16 | 9 | 56.3 |
| | **JUMLA** | **61** | **50** | 82.0 |

**Kiambatisho Nam. 2. Orodha ya Mada zilijadiliwa kupitia Televisheni na Redio katika kipindi cha "Unatekelezaje?" kwa Mwaka wa fedha Julai 2021 - Machi 2022.**

## Mwezi Julai 2021

| Nam. | Muhusika | Mada iliyojadiliwa | Siku iliyorikodiwa | Siku ya iliyorushwa hewani ZCTV | Siku iliyorushwa hewani ZBC TV |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" - Mhe Hamida Mussa Khamis | Utekelezaji wa maagizo ya Mhe Rais | Ijumaa 25/06/2021 | Alhamis 01/07/2021 | Jumapili 04/07/2021 |
| 2 | Mhadhiri - Idara ya Habari na Mawasiliano ya Umma Dkt Saleh Koshuma | Tathmini ya ziara ya Mkoa wa Kusini Unguja | Alhamis 08/07/2021 | Alhamis 08/07/2022 | Jumapili 11/07/2021 |
| 3 | Mchamuzi wa Siasa na Maendeleo ya Jamii - Nd Mohamed Mohamed Abdalla Mohamed | Mambo 10 - Majumuisho ya Ziara ya Mjini Magharibi | Alhamis 22/07/2021 | Alhamis 22/07/2022 | Jumapili 01/08/2021 |
| 4 | Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) Nd Jamila Mahamoud Juma | Kongamano la kutokomeza Udhalilishaji Zanzibar | Alhamis 29/07/2021 | Alhamis 29/07/2021 | Jumapili 01/08/2021 |
| **Mwezi Agosti 2021 – 2022** | | | | | |

| Nam. | Muhusika | Mada iliyojadiliwa | Siku iliyorikodiwa | Siku ya iliyorushwa hewani ZCTV | Siku iliyorushwa hewani ZBC TV |
|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Mkurugenzi Baraza la Utoaji wa Leseni Zanzibar Nd Rashid Ali Salim | Utekelezaji wa jumla wa Baraza la Leseni | Jumatano 04/07/2021 | Alhamis | Jumapili 15/08/2021 |
| 7 | Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba - Nd Mwanaisha Ali Said | Utekelezaji wa Mipango ya Shirika | Alhamis 19/08/2021 | Alhamis 19/08/2022 | Jumapili 22/08/2021 |
| 8 | Mkurugenzi Mtendaji, Jumuiya ya Kitaifa ya Wafanyabiashara Zanzibar – ZANDIAS | Umuhimu wa sekta binafsi katika Ukuaji wa Uchumi | Ijumaa 20/06/2021 | Alhamis 26/08/2021 | Jumapili 29/08/2021 |
| **Mwezi Septemba 2021** | | | | | |
| 9 | Mkurugenzi, Idara ya Usalama Kazini | Utekelezaji wa jumla | Jumatano 01/09/2021 | Alhamis 02/09/2021 | Jumapili 05/09/2021 |
| 10 | Afisa Mawasiliano Shieika la Umeme Zanzibar - ZECO Juma Haji Juma (Chapa) | Utekelezaii wa maagizo ya Mheshimiwa Rais Kiongwe | 9/16/2021 | 9/16/2021 | 9/17/2021 |

| Nam. | Muhusika | Mada iliyojadiliwa | Siku iliyorikodiwa | Siku ya iliyorushwa hewani ZCTV | Siku iliyorushwa hewani ZBC TV |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 | Afisa Uhusiano Mamlala ka Usafiri na Usalama Barabarani Nd Hakim Daudi Mwita, Katibu wa Jumuiya ya Bodaboda Zanzibar Ali Salim Kibwanga | Urasimishaji wa usafiri wa Boda boda na Bajaji | Alhamis 23/09/2021 | Alhamis 23/09/2021 | Jumapili 26/09/2021 |
| 13 | Mkurugenzi Mipango Sera na Utafiti TAMISEMIM Nd Abdulla Issa Mgongo | Uzinduzi wa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo | Jumatano 29/09/2021 | Alhamis 30/09/2021 | Jumapili 03/10/2021 |
| **Mwezi Oktoba 2021** | | | | | |
| 14 | Mkuu wa Divisheni ya Mazingira Manispaa ya Magharibi 'A' Bi. Asha Salum Bakari na Afisa Mazingira Mwl. Ali Juma Machano | Utekelezaji wa Maagizo na Ahadi za Mhe. Rais | Alhamis 14/10/2021 | Alhamis 14/10/2022 | Jumapili 17/10/2021 |
| 15 | Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Haroun Ali Suleiman | Kuelekea Maadhimisho ya Mwaka Mmoja wa Rais Dk. Mwinyi - Utekelezaji wa Maagizo na Ahadi za Mhe. Rais | Jumanne 19/10/2021 | Alhamis 21/10/2021 | Jumapili 24/10/2021 |

| Nam. | Muhusika | Mada iliyojadiliwa | Siku iliyorikodiwa | Siku ya iliyorushwa hewani ZCTV | Siku iliyorushwa hewani ZBC TV |
|---|---|---|---|---|---|
| 16 | Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Khalid | Kuelekea Maadhimisho ya Mwaka Mmoja wa Rais Dk. Mwinyi - Utekelezaji wa Maagizo na Ahadi za Mhe. Rais | Jumatano 27/10/2021 | Alhamis 28/10/2021 | Jumapili 31/10/2021 |
| **Mwezi Novemba 2021** | | | | | |
| 17 | Mkurugenzi Idara ya Elimu ya Msingi Nd. | Utekelezaji wa Majukumu wa Idara ya Elimu ya Msingi | Alhamis 28/10/2021 | Alhamis 04/11/2021 | Jumapili 07/11/2021 |
| 19 | Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Mhe. Leila Mahamoud Mussa | Utekelezaji wa mwaka mmoja wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | Jumanne 16/11/2021 | Alhamis 18/11/2021 | Jumapili 21/11/2021 |
| **Mwezi Disemba 2021** | | | | | |
| 20 | Mwanasheria (ZPDC) Walid Mohamed Adam | Gesi na Mafuta | Alhamis 02/12/2021 | Alhamis 02/12/2022 | Jumapili 05/12/2021 |
| 21 | Mhe. Suleiman Masoud Makame | Waziri wa Maji, Nishati na Madini | Ijumaa 10/12/2021 | Alhamis 16/12/2021 | Jumapili 19/12/2021 |
| 22 | Idara ya Mawasiliano Ikulu | Taarifa za Mkutano wa Mhe. Rais na wahariri na waandishi wa Habari | Alhamis 23/12/2021 | Alhamis 23/12/2022 | Jumapili 26/09/2021 |

| Mwezi Januari 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 23 | Makala maalumu ya ZAWA | Maendeleo ya Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar – ZAWA | | | |
| **Nam.** | **Muhusika** | **Mada iliyojadiliwa** | **Siku iliyorikodiwa** | **Siku ya iliyorushwa hewani ZCTV** | **Siku iliyorushwa hewani ZBC TV** |
| 23 | Nd. Zuhura Saleh Amour - Mratibu wa Kitengo cha Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU , Nd. Bakari Hamad Magarawa - Meneja wa Kitendo cha Elimu ya Afya kwa Umma | Taarifa za Uzinduzi wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation | Jumatano 02/03/2022 | Alhamis 03/03/2022 | Jumapili 06/03/2022 |
| 24 | Nd. Adam Abdullah Makame - Mkurugenzi Mwendeshaji ZPRA, Nd. Arafa Salim Rashid – Mwanasheria | Utekelezaji wa Malamka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia | Jumatano 09/03/2022 | Alhamis 10/03/2022 | Jumapili 13/03/2022 |
| 25 | Nd. Abdalla Mohamed Mussa - Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Elimu, Zanzibar | Utekelezaji wa Taasisi ya Elimu - Matayarisho ya Mitaala ya Skuli za Maandalizi na Msingi | Alhamis 17/03/2022 | Alhamis 17/03/2023 | Jumapili 20/03/2022 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 25 | Idara ya Mawasiliano Ikulu | Makala Maalumu ya Utekelezaji wa ahadi za Taasisi ya ZMBF | Alhamis 31/03/2023 | Alhamis 31/03/2024 | Jumapili 03/04/2022 |

**Kiambatisho Nam. 3. Idadi ya taarifa zilizorushwa na waliotembelea Tovuti ya Ikulu kwa Kipindi cha Miezi Tisa 2021 – 2022**

| KIPINDI CHA WAKATI | MWEZI | IDADI YA TAARIFA | IDADI WALIOTEMBELEA TOVUTI |
|---|---|---|---|
| ROBO YA KWANZA | JULAI | 68 | 5,380 |
| | AGOSTI | 28 | 5,496 |
| | SEPTEMBA | 30 | 7,248 |
| ROBO YA PILI | OKTOBA | 49 | 7,691 |
| | NOVEMBA | 73 | 22,236 |
| | DISEMBA | 34 | 5,518 |
| ROBO YA TATU | JANUARI | 76 | 5,244 |
| | FEBUARI | 41 | 3,636 |
| | MACHI | 49 | 4,540 |
| **JUMLA** | | **448** | **66,989** |

**Kiambatisho Nam. 4. Taarifa zilizorushwa Kupitia Mitandao ya Kijamii ya Ikulu Kipindi cha Miezi Tisa 2021 – 2022.**

| KIPINDI CHA WAKATI | JINA LA MTANDAO | MATUKIO | IDADI WATU WALIOTEMBELEA TOVUTI |
|---|---|---|---|
| ROBO YA KWANZA | FACEBOOK | 129 | 53,009 |
| | INSTAGRAM | 150 | 94,109 |
| | WHATSAPP | 170 | 2,224 |
| | TWITTER | 88 | 19,801 |
| | TIKTOK | - | - |
| ROBO YA PILI | FACEBOOK | 127 | 61,154 |
| | INSTAGRAM | 135 | 127,125 |
| | WHATSAPP | 189 | 2,330 |
| | TWITTER | 30 | 22,134 |
| | TIKTOK | - | - |
| ROBO YA TATU | FACEBOOK | 184 | 65,235 |
| | INSTAGRAM | 138 | 174,321 |

| KIPINDI CHA WAKATI | JINA LA MTANDAO | MATUKIO | IDADI WATU WALIOTEMBELEA TOVUTI |
|---|---|---|---|
| | WHATSAPP | 203 | 2,352 |
| | TWITTER | 113 | 29,302 |
| | TIKTOK | 121 | 23,300 |
| **JUMLA** | | **1,777** | **676,396** |

**Kiambatisho Nam. 5. Orodha ya Malalamiko yaliyowasilishwa na Wananchi kwa Kipindi cha Miezi 9 kutoka Julai mpaka Machi 2021/2022.**

| Mwezi | Jumla ya Malalamiko (Mawasilisho) | Malalamiko yaliyopatiwa Ufumbuzi | Malalamiko yanayofuatiliwa | Asilimia ya Malalamiko yaliyopatiwa Ufumbuzi |
|---|---|---|---|---|
| Julai | 370 | 149 | 221 | 40.3 |
| Agosti | 411 | 237 | 174 | 57.7 |
| Septemba | 312 | 190 | 122 | 60.9 |
| Octoba | 208 | 176 | 32 | 84.6 |
| Novemba | 234 | 211 | 23 | 90.2 |
| Disemba | 219 | 197 | 22 | 90.0 |
| January | 347 | 197 | 150 | 56.8 |
| Febuari | 310 | 270 | 40 | 87.1 |
| Machi | 416 | 400 | 16 | 96.2 |
| **JUMLA** | **2,827** | **2,027** | **800** | **71.7** |

**Kiambatisho Nam. 6. Takwimu za Malalamiko yaliyowasilishwa na Wananchi kwa Taasisi 45 za Serikali Zilizounganishwa katika Mfumo wa Sema na Rais kwa Kipindi Julai – Machi 2021/2022.**

| Nam. | Jina la Taasisi | Jumla ya Malalamiko | Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi | Malalamiko yanayofuatiliwa | Asilimia ya Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango | 83 | 70 | 13 | 84.3 |
| 2 | Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) | 47 | 45 | 2 | 95.7 |
| 3 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) | 43 | 41 | 2 | 95.3 |
| 4 | Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) | 32 | 31 | 1 | 96.9 |
| 5 | Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) | 5 | 5 | 0 | 100.0 |
| 6 | Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | 47 | 36 | 11 | 76.6 |
| 7 | Tume ya Utumishi Serikalini | 42 | 40 | 2 | 95.2 |
| 8 | Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | 25 | 18 | 7 | 72.0 |
| 9 | Wakfu na Mali ya Amana | 25 | 24 | 1 | 96.0 |

| **Nam.** | **Jina la Taasisi** | **Jumla ya Malalamiko** | **Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi** | **Malalamiko yanayofuatiliwa** | **Asilimia ya Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi** |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar | 28 | 16 | 12 | 57.1 |
| 11 | Mahakama Kuu ya Zanzibar | 130 | 124 | 6 | 95.4 |
| 12 | Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi, na Uwekezaji | 128 | 100 | 28 | 78.1 |
| 13 | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ | 300 | 277 | 23 | 92.3 |
| 14 | Wakala wa Usajili wa matukio ya Kijamii Zanzibar | 45 | 45 | 0 | 100.0 |
| 15 | Baraza la Manispaa Mjini | 72 | 41 | 31 | 56.9 |
| 16 | Baraza la Manispaa Magharibi A | 12 | 7 | 5 | 58.3 |
| 17 | Baraza la Manispaa Magharibi B | 57 | 43 | 14 | 75.4 |
| 18 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba | 16 | 8 | 8 | 50.0 |
| 19 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba | 18 | 14 | 4 | 77.8 |
| 20 | Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais | 12 | 9 | 3 | 75.0 |
| 21 | Idara ya Watu wenye Ulemavu | 21 | 16 | 5 | 76.2 |
| 22 | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi | 38 | 33 | 5 | 86.8 |

| Nam. | Jina la Taasisi | Jumla ya Malalamiko | Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi | Malalamiko yanayofuatiliwa | Asilimia ya Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| 23 | Wizara ya Uchumi wa buluu na Uvuvi | 22 | 17 | 5 | 77.3 |
| 24 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | 12 | 7 | 5 | 58.3 |
| 25 | Kamisheni ya Utalii Zanzibar | 19 | 16 | 3 | 84.2 |
| 26 | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | 60 | 58 | 2 | 96.7 |
| 27 | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo | 37 | 34 | 3 | 91.9 |
| 28 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 243 | 66 | 177 | 27.2 |
| 29 | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar | 50 | 32 | 18 | 64.0 |
| 30 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 67 | 54 | 13 | 80.6 |
| 31 | Kamisheni ya Ardhi | 70 | 40 | 30 | 57.1 |
| 32 | Wizara ya Biashara, Maendeleo ya Viwanda. | 75 | 63 | 12 | 84.0 |
| 33 | Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto | 186 | 148 | 38 | 79.6 |
| 34 | Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja | 91 | 70 | 21 | 76.9 |
| 35 | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 145 | 62 | 83 | 42.8 |
| 36 | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar | 36 | 31 | 5 | 86.1 |

| Nam. | Jina la Taasisi | Jumla ya Malalamiko | Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi | Malalamiko yanayofuatiliwa | Asilimia ya Malalamiko yaliyopatiwa ufumbuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| 37 | Shirika la Bandari Zanzibar | 12 | 10 | 2 | 83.3 |
| 38 | Wizara ya Maji, Nishati na Madini | 9 | 6 | 3 | 66.7 |
| 39 | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | 126 | 80 | 46 | 63.5 |
| 40 | Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | 150 | 89 | 61 | 59.3 |
| 41 | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za maji na Nishati Zanzibar | 9 | 6 | 3 | 66.7 |
| 42 | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) | 17 | 15 | 2 | 88.2 |
| 43 | Idara ya Uhamiaji Zanzibar | 24 | 21 | 3 | 87.5 |
| 44 | Jeshi la Polisi | 136 | 54 | 82 | 39.7 |
| 45 | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 5 | 5 | 0 | 100.0 |

**Kiambatisho Nam. 7. Idadi ya Taasisi na Watumishi waliopatiwa Semina ya Utunzaji Nyaraka na Udhibiti wa Siri za Serikali.**

| NAM. | JINA LA WIZARA/TAASISI | IDADI |
|---|---|---|
| 1 | WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA (ZICTIA) | 37 |
| 2 | WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI | 32 |
| 3 | SEKRETARIET YA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA-ZANZIBAR | 3 |
| 4 | WAKALA WA UCHAPAJI WA SERIKALI (Semina maalum kwa washiriki wa zoezi la uchapaji na uhifadhi wa mitihani ya Taifa) | 83 |
| 5 | TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU PEMBA | 23 |
| 6 | WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI PEMBA | 24 |
| | **JUMLA** | **202** |

**Kiambatisho Nam. 8. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Kazi za Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023.**

| NAM. | PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | BAJETI KWA MWAKA WA 2021/2022 | FEDHA ZLIZOPATIKANA 2021/2022 | ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA | MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Program Kuu ya Kusimamia na Kuratibu Shughuli na Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu. | Programu Ndogo ya Kusimamia huduma na shughuli za Mheshimiwa Rais. | 3,441,945,500 | 2,001,933,477 | 58.2 | 4,610,043,000 |
| | | Programu Ndogo ya Kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi | 536,071,170 | 167,853,726 | 31.3 | 998,371,000 |
| | | Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miradi ya Kimkakati ya Serikali. | - | - | - | 300,000,000 |
| | **JUMLA YA PROGRAMU KUU** | | **3,978,016,670** | **2,169,787,203** | | **5,908,414,000** |
| 2 | Programu Kuu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi. | Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kikanda na Kimataifa. | 801,669,440 | 187,619,679 | 23.4 | 441,533,000 |
| | | Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli za Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. | | | | 487,661,000 |
| | **JUMLA YA PROGRAMU KUU** | | **801,669,440** | **187,619,679** | | **929,194,000** |

| NAM. | PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | BAJETI KWA MWAKA WA 2021/2022 | FEDHA ZLIZOPATIKANA 2021/2022 | ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA | MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Program Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Afisi ya Rais Ikulu. | Programu Ndogo ya Uratibu na usimamizi wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu. | 368,000,000 | 77,885,790 | 21.2 | 1,597,336,000 |
| | | Programu Ndogo ya Uratibu wa shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Afisi ya Rais Ikulu | 150,000,000 | 35,753,225 | 23.8 | 398,895,000 |
| | | Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa shughuli za Afisi ya Rais Ikulu Pemba. | 322,400,000 | 98,925,900 | 30.7 | 1,189,133,000 |
| | | Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama wa watumishi wa Umma. | 270,666,000 | 29,201,768 | 10.8 | 320,000,000 |
| | **JUMLA YA PROGRAMU KUU** | | **1,111,066,000** | **241,766,683** | | **3,505,364,000** |
| 4 | Program Kuu ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka. | Programu Ndogo ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka. | 574,294,448 | 318,404,075 | 55.4 | 758,566,000 |
| | **JUMLA YA PROGRAMU KUU** | | **574,294,448** | **318,404,075** | | **758,566,000** |

| NAM. | PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | BAJETI KWA MWAKA WA 2021/2022 | FEDHA ZLIZOPATIKANA 2021/2022 | ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA | MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | Programu ya Uratibu wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi. | Uratibu wa Shughuli za BLM na Majukumu ya KBLM/KMK. | 633,450,000 | 168,081,400 | 26.5 | 764,190,000 |
| | | Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi wa Taasisi za Umma. | 53,750,000 | 10,140,000 | 18.9 | 54,550,000 |
| | **JUMLA YA PROGRAMU KUU** | | **687,200,000** | **178,221,400** | | **818,740,000** |
| 6 | Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi. | Programu Ndogo ya Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi. | 1,507,300,000 | 1,003,552,835 | 66.6 | 1,615,760,000 |
| | **JUMLA YA PROGRAMU KUU** | | **1,507,300,000** | **1,003,552,835** | | **1,615,760,000** |
| | **JUMLA YA PROGRAMU KUU KWA FUNGU A01 NA A02** | | **8,659,546,558** | **4,099,351,875** | **47** | **13,536,038,000** |